# Class 7 mid-term 1 August 2021 Kiswahili

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.***

____1____ ziwa Fahari, tuliwaona mamba wakubwa ajabu, ____2_____ kando yao. Wote walijipasha joto ____3____ mwamba ____4____ uliokuwa ____5____ na ____6____. Mwalimu Kazungu alitufahamisha kuwa nyama yao ni ____7_____ mno. Kwa woga. ____8____ yetu ilidunda dududu! Kusema kweli, sura zao ____9____ sana.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. Tulivyofika | B. Tulipofika | C. Tulipowadia | D. Tulivyosafiri |
| **2.** | A. vigwena | B. vichengo | C. visui | D. vivinimbi |
| **3.** | A. chini ya | B. katikati ya | C. juu ya | D. kati ya |
| **4.** | A. kubwa | B. refu | C. dogo | D. mkubwa |
| **5.** | A. mbali | B. mbele | C. kando | D. karibu |
| **6.** | A. ufuo | B. utepe | C. maji | D. mto |
| **7.** | A. mtamu | B. ghali | C. mchungu | D. mzuri |
| **8.** | A. mioyo | B. moyo | C. roho | D. nyoyo |
| **9.** | A. zilipendeza | B. zilionekana | C. ziliogofya | D. zilivutia |

Hapo ____10____, wanafunzi walikuwa wakipewa ____11____ kalikali wakikosa. Mwanafunzi ____12____ sikioni au mkononi au kuchapwa makalioni. Njia ____13____ ilipigwa marufuku na serikali na mtindo wa mashauriano ukachukuliwa. Hata hivyo, wanafunzi wanapaswa ____14____ wakiwa na mwelekeo ____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. samani | B. zamani | C. shule | D. shuleni |
| **11.** | A. adabu | B. dhahabu | C. viboko | D. adhabu |
| **12.** | A. angefinywa | B. angechunwa | C. angegwarwa | D. angetwangwa |
| **13.** | A. hilo | B. lile | C. hiyo | D. yale |
| **14.** | A. wakuwe | B. wakuue | C. wauawe | D. wakue |
| **15.** | A. mwema | B. mema | C. jema | D. njema |

***Kutoka nambari 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo.***

**16.** Chagua jina lililo tofauti na mengine.
A. Ubawa B. Bilauri
C. Mbuzi D. Seredani

**17.** Bainisha kielezi katika sentensi hii:
**Wanafunzi watano walikimbia kwa kasi.**
A. Watano
B. Walikimbia
C. Kwa kasi
D. Wanafunzi

**18.** Nomino hizi hupatikana katika ngeli gani?
***Ugonjwa, ulezi, upishi***
A. LI - YA B. U - U
C. U - I D. U - YA

**19.** Chagua sentensi yenye **KI** ya udogo.
A. Kiambaza kile kitapakwa rangi.
B. Kitoto chenyewe kinaugua unyafuzi.
C. Alicheza kishujaa akatuzwa.
D. Ukisoma kwa bidii utafaulu katika mtihani.

**20.** Chagua neno ambalo **si** aina ya vazi.
A. Gagro
B. Shimizi
C. Buibui
D. Vuli

**21.** Ni upi wingi wa:
**Ulikila chakula chako?**
A. Ulikula vyakula vyenu?
B. Ulivila vyakula vyako?
C. Mlivila vyakula vyenu?
D. Ulikula vyakula vyenu?

**22.** Tegua kitendawili hiki:
**Ziwa la kwetu twaogelea kando kando,**
A. upepo
B. maji
C. mbingu na nyota
D. moto

**23.** Bata ni kwa kiyoyo kama vile nyuki ni kwa
A. buu B. kinda
C. jana D. kinyemere

**24.** Kanusha sentensi ifuatayo:
**Maembe yote yameoza.**
A. Maembe yote hayajaoza.
B. Maembe yote hayakuoza.
C. Maembe yote hayaozi.
D. Maembe yote hayataoza.

**25.** $^1/_6$ kwa maneno huitwaje?
A. Tusui
B. Sudusi
C. Thumni
D. Khumusi

**26.** Chagua wingi wa:
**Mjusi ameliwa na joka.**
A. Wajusi wameliwa na majoka.
B. Mijusi wameliwa na nyoka.
C. Mijusi wameliwa na majoka.
D. Wajusi wameliwa na nyoka.

**27.** Chagua methali yenye maana sawa na:
**Kuchumbia si kuoa.**
A. Majuto ni mjukuu.
B. Kulenga si kufuma.
C. Haraka haraka haina baraka.
D. Bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi.

**28.** Ni ipi **si** aina ya shairi?
A. Tarbia B. Takhmisa
C. Tathlitha D. Kibwagizo

**29.** Chagua usemi wa taarifa wa:
**"Ukikimbia gizani utaanguka," mama alimwambia mwanawe.**
A. Mama alimwambia mwanawe kuwa akikimbia gizani ataanguka.
B. Mama aliwaambia wanawe kuwa wangekimbia gizani wangeanguka.
C. Mama alimwambia mwanawe kuwa angekimbia gizani angeanguka.
D. Mama alimwambia mwanawe kuwa ukikimbia gizani utaanguka.

**30.** Kisawe cha **wiki** ni
A. mwongo B. mwaka
C. mwezi D. juma

***<u>Soma kifungu kifuatacho, kisha ujibu swali la 31 hadi 40.</u>***

Jana nilipomaliza kula **<u>chakula cha jioni</u>**, nilienda katika chumba changu cha kulala. Kwa vile nilikuwa nikiona usingizi sana, nilijilaza kitandani na **<u>kujifunika gubigubi</u>** kwa blanketi.

Hivyo ndivyo nilivyosafiri katika dunia nyingine kabisa. Nilianza kutembea hapa na pale bila mpango maalumu. Katika tembeatembea hizo, nilikutana na joka kubwa jeusi kuliko hata makaa. Joka hilo lilikuwa likitokwa na jasho na ulimi wake mkubwa ulikuwa umejianika nje. Woga ulionishika ulifanya miguu yangu kuanza kutetemeka na nikajipata nikijiendeshea.

Joka hilo lilianza kunikaribia polepole. Mimi huyo! Nikatimua mbio kwa kasi kama duma huku joka hilo likinifuata kwa tamaa ya kunikamata na kunifanya kitoweo. Mara, lo! Huko nilikokuwa nikielekea nilimwona simba mkubwa. Simba huyo aliponiona, naye akamshukuru Mungu kwa kumletea chakula kwa njia rahisi hivyo.

Nilishindwa nifanye nini. Mbele kulikuwa na simba na nyuma joka. Sikuzubaa. Nilifanya akili mara moja. Niliupanda mti uliokuwa karibu nami. Joka hilo lilinifuata hadi kwenye mti huo. Lilipanda polepole huku likinikodolea macho, nami nikabaki kufanya maombi yangu ya mwisho. Naye simba alikuwa pale chini akiniangalia na kunguruma kwa sauti akiningojea niteremke.

Maskini mimi! Joka lile lilipokuwa tu lanifikia, tawi nililokuwa nimekalia likakatika. Mimi huyo! Nikajibwaga chini pu! Kama gunia la mawe. Punde si punde, niliamka hapo chini mbio kama aliyerukwa na akili. Simba akanifuata nyuma kwa kasi ya mshale. Aliponikaribia na kulifumbua domo lake kubwa kunimeza mzimamzima, niligutuka usingizini na kujipata nikitokwa na jasho kwelikweli. Alhamdulilahi! Nilifurahi sana kwamba ilikuwa ndoto tu.

**31.** Ni kwa nini mwandishi alienda kulala moja kwa moja? Alikuwa
A. ameshiba sana
B. amechoka sana
C. na usingizi mwingi
D. amekasirika sana

**32.** <u>**Chakula cha jioni**</u> ni sawa na
A. kiamshakinywa
B. chamcha
C. kijio
D. kishuka

**33.** Katika ndoto yake, mwandishi aliona
A. joka kubwa
B. nyoka mdogo
C. nyoka mweupe
D. nyoka mfupi

**34.** Mwandishi alipomwona nyoka, alianza
A. kucheka
B. kulia
C. kutetemeka
D. kukimbia

**35.** Joka lilipoanza kumkaribia mwandishi,
A. alijitayarisha kupambana nalo.
B. alitoroka mbio
C. alikata tamaa
D. aligutuka na kuamka

**36.** <u>**Kujifunika gubigubi**</u> ni mfano wa
A. tanakali ya sauti
B. tashbihi
C. istiara
D. nahau

**37.** Ni upi mfululizo sahihi wa matukio?
A. Kula, kulala, kuota, kuamka
B. Kula, kuota, kulala, kuamka
C. Kuota, kula, kulala, kuamka
D. Kulala, kuota, kuamka, kula

**38.** Kwa jumla, msimulizi alikabiliwa na hatari ngapi?
A. Nne
B. Tatu
C. Mbili
D. Moja

**39.** Msimulizi aliamka usingizini wakati gani?
A. Usingizi ulipomwishia.
B. Simba alipopanua mdomo.
C. Alipoamshwa asubuhi.
D. Wanyama walipomwacha.

**40.** Kichwa kifaacho **zaidi** taarifa hii ni
A. Simba mkali
B. Nyoka wa kutisha
C. Ndoto ya kutisha
D. Usingizi wa ajabu.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.</u>***

Sokoni ni mahali pa shughuli <u>**anuwai**</u>. Miongoni mwa shughuli hizi nyingi, iliyo dhahiri ni ya uuzaji na ununuzi wa bidhaa. Wafanyabiashara husafirisha bidhaa zao kutoka sehemu mbalimbali kupeleka sokoni. Aghalabu kila sehemu huwa na siku mahususi katika wiki ambayo imetengwa kwa minajili ya soko. Siku hii, shughuli hunoga kwelikweli.

Ili shughuli zitiririke barabara, upo mpangilio maalumu ambao huzingatiwa na wauzaji wote. Jambo hili hurahisisha upataji wa bidhaa kwa urahisi, hivyo mteja hataharibu muda wake akirandaranda hapa na pale akibahatisha kuwapo kwa bidhaa fulani.

Matunda na aina fulani za mboga zimetengewa vibanda vyao ili anayehitaji matunda tofauti tofauti aweze kuyapata katika sehemu moja. Wanaouza nafaka wana sehemu zao pia. Sehemu yenye kelele nyingi ni ile ambapo **mavulia** huuzwa. Hapa, kila muuzaji wa nguo hizi hutumia lugha yenye mnato na ucheshi. Kusudi lake huwa ni kuwavutia wanunuzi. Wao wana maneno matamu ya kumtoa nyoka pangoni. **Ni nadra kukosa kioja hapa**. Unaweza kumwona mwanamume mzima amevalia mavazi ya kike kwa nia ya kuwavutia kina dada ambao ndio wateja wakuu wa bidhaa zake.

Zipo sehemu maalumu ambazo zimetengewa wauzaji wa mifugo. Wanaokusudia kununua mitamba na mifarika huwapata hapa. Asubuhi na mapema, wanunuzi hufurika hapa huku kila mmoja akiwa na uchu wa kufanikiwa kupata bidhaa bora. Wauzaji nao hudhamiria kupata faida kubwa.

Kuna kikundi cha wafanyabiashara ambacho hakitulii mahali pamoja. Wanaojipatia riziki kwa njia hii, **hupiga milundi** kutoka upande mmoja wa soko hadi mwingine. Msimu wa kiangazi, utawaona wakitiririkwa na kijasho, nayo masika huja na madhila yake. Ifikapo jioni, utawaona wavutao mikokoteni na pitapita zao za hapa na pale. Wapagazi nao hawaachwi nyuma. Hakika, masoko huchangia pakubwa katika kuzipa familia nyingi mkate wa kila siku.

---

**41.** Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kusema
A. shughuli za sokoni ni chache sana.
B. shughuli kubwa sokoni ni ya uuzaji na ununuzi.
C. bidhaa nyingi hukuzwa sokoni.
D. shughuli za sokoni huanza polepole.

**42.** Ni dhahiri kuwa
A. kuna siku maalumu ya kufanya uuzaji na ununuzi katika kila eneo.
B. wanunuzi huharibu muda mwingi wakirandaranda.
C. bidhaa zote sokoni hupatikana katika eneo moja.
D. wauzaji wote huwa na bidhaa zinazofanana.

**43.** Mwandishi amesema mpangilio mzuri wa bidhaa sokoni huwezesha
A. uuzaji wa haraka
B. utembeaji wa haraka
C. wepesi wa kupata bidhaa
D. udumishaji wa sheria

**44.** Kulingana na kifungu, manufaa ya kuuzia matunda na mboga pamoja ni kuwa
A. mnunuzi hatatembea sana
B. bei ya matunda na mboga ni nafuu
C. kuna vibanda vilivyo salama.
D. mnunuzi ana nafasi ya kupata chaguo lake mahali pamoja.

**45.** Mwandishi wa kifungu anasema lugha yenye ucheshi na mnato mara nyingi hutumiwa na
A. wanaouza mboga na matunda.
B. wanaouza nguo kuukuu.
C. wanaosukuma mikokoteni.
D. wauzaji wa nafaka.

**46.** "**Ni nadra kukosa kioja hapa**" ndiko kusema kuwa
A. kila mara kuna vioja vingi.
B. ni vigumu sana kuona kioja hapa.
C. si rahisi kukosa kioja hapa.
D. vioja hapa ni tele.

**47.** Kwa maoni yako, **mavulia** ni aina ya
A. wanyama B. nguo
C. nafaka D. matunda

**48.** Katika aya ya mwisho, mwandishi anawarejelea kina nani?
A. Wajuzi B. Wachuuzi
C. Madalali D. Wazegazega

**49.** **....anuwai....** ni sawa na
A. chache B. uuzaji na ununuzi
C. aghalabu D. tofauti tofauti

**50.** Maana ya **hupiga milundi** ni
A. hutembea kwa miguu
B. hutoroka hatari.
C. huenda haraka haraka.
D. hutembea asteaste.